

HALMASHAURI YA MJI WA IFAKARA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji)



Simu: 023 - 2931523
Fax: 023 - 2931513
E-mail : info@ifakaradc.go.tz
www.ifakaradc.go.tz

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji,
S. L P. 433,
IFAKARA

TAARIFA KWA UMMA. MACHINJIO YA NG'OMBE KAPORO YAFUNGULIWA BAADA YA UKARABATI KUKAMILIKA.

Halmashauri ya Mji Ifakara inapenda kuwataarifu Wananchi wake kuwa Machinjio ya Ng'ombe iliyopo Kaporo Mjini Ifakara ambayo ilikuwa imefungwa kwa siku mbili kuanzia tarehe **04.04.2017** kwa ajili ya ukarabati mdogo imefunguliwa leo tarehe **06.4.2017** baada ya ukarabati huo kukamilika na hivyo kukidhi vigezo na masharti ya Afya za Walaji wa nyama.

Hivyo tunapenda Umma utambue kuwa huduma ya uuzaji wa nyama mabuchani imerejea kama kawaida na hivyo hakuna tena upungufu wala ukosefu wa nyama Mjini Ifakara.

Fatna Mfalingundi,
**AFISA HABARI NA UHUSIANO,
HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.
06.04.2017**

